

# IKULU ZANZIBAR



## SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 024

ISSN 1821 - 8253

MACHI - APRILI 2016



**Wananchi wa Zanzibar wameamua**  
**■ Wamemchagua tena Dk. Shein kuwa Rais**

# Bodi ya Wahariri

## Mhariri Mkuu

Hassan K. Hassan

## Mhariri Msaidizi

Ali S. Hafidh

## Waandishi

Said J. Ameir

Rajab Y. Mkasaba

Haji M. Ussi

Said K. Salim

Yunus S. Hassan

Mahfoudha M. Ali

Amina M. Ameir

## Mpiga Picha

Ramadhan O. Abdalla

## Msanifu

Aziz I. Suwed

# UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudhi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.

Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.BOX: 2422

Zanzibar - Tanzania

Phone: +255 223 081/5

Fax: 024 223 3722

Email: com\_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz

# Maoni ya Mhariri

## Muelekeo wetu uwe kuleta maendeleo endelevu

**W**ananchi wa Zanzibar pamoja na wenzao wa Tanzania Bara wanastahiki kujipongeza kufuatia kumalizika kwa salama, amani na utulivu kwa uchaguzi mkuu ambao ni moja kati ya majukumu muhimu ya kikatiba na kidemokrasia. Hatua hiyo imeliwezesha taifa kupata viongozi halali waliochaguliwa na wananchi kuiongoza nchi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Uzoefu wa Tanzania, Barani Afrika na kwengineko duniani, kipindi cha uchaguzi ndicho kipindi pekee chenyehis za watu wengi wakiwemo wanasiwa na wanajamii wa rika na jinsia tofauti. Katika kipindi hiki wanasiwa hutumia njia za aina mbali mbali kuwashawishi wananchi kuwapigia kura kuititia vyama vyao vya siasa au njia nyengine zozote.

Harakati za siasa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu huambatana na mambo mengi ikiwemo takrima, vitisho, kuchafuliana majina kwa lengo la kushushiana hadhi mbele ya jamii na kujitafutia njia za kupata ushindi. Lakini kubwa zaidi ni wasi wasi juu ya uwezekano wa kuvunjika kwa hali ya amani na utulivu hasa kwa nchi kama Tanzania, ambayo kwa muda mrefu imekuwa ndiyo darasa la kujifunza amani mbele ya mataifa mengine duniani.

Kutokana na hali hiyo ya wasi wasi, baadhi ya mataifa duniani na mashirika yanayoshughulikia kusafirisha watu kibiaresha au kiutalii yamekuwa yakitoa indhari kwa wananchi na wateja wao wanapopanga kuzitembelea nchi ambazo katika kipindi hicho zinafanya uchaguzi. Hatua hiyo hupelekea nchi husika kuwa na upungufu mkubwa wa watalii katika kipindi cha uchaguzi.

Katika kukabiliana na athari ambazo zingeweza kutokea kabla, wakati na baada ya uchaguzi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ziliwahakikisha wananchi pamoja na washirika wa maendeleo kwamba uchaguzi utakuwa wa amani, huru na wa haki na kwamba kila mtu atapata kuitumia haki yake ya kupiga kura bila ya usumbu孚 wowote.

Pamoja na kuripotiwa baadhi ya dosari zilizopelekea kufutwa kwa uchaguzi wa Zanzibar wa tarehe 25 Oktoba, 2015, uchaguzi wa marudio wa tarehe 20 Machi, 2016, ulifanyika kwa mafanikio makubwa na kila mwananchi alipata kutumia haki yake ya kumchagua kiongozi aliyemtaka.

Ni dhahiri kwamba kuna kila sababu kwa Watanzania na hasa Wazanzibari kujipongeza kwa hatua hiyo ambayo sio watu

wengi waliorajia kwamba ingemalizika kwa amani, utulivu na usalama kama ilivyotokea. Hii kwa Mara nyengine ilidhahirisha namna Wazanzibari walivyokomaa kisiasa na kufahamu maana halisi ya amani na athari za uvunjifu wa amani.

Kuna msemo wa kiswahili usemao "iliyopitayo si ndwele, tugange ijayo". Wakati umefika sasa kwa wananchi wote kuona haja, umuhimu au ulazima wa kuendeleza harakati za kuleta maendeleo endelevu badala ya kuendelea kukaa vijiwi kuzungumzia siasa ambazo wakati wake umeshamalizika.

Ni ukweli uliowazi kwamba hivi sasa kumekuwa na fursa nydingi za kuweza kujikwamua na umasikini iwapo kila mtu ataamua kufanyakazi kwa bidii. Serikali imeshafanya juhudi kubwa za kueneza huduma za maji safi na salama vijijini, umeme na mtatandao wa barabara za lami.

Sekta ya kilimo imeimarishwa sana kwa kuinua hadhi taasisi ya utafiti ya Kizimbani pamoja na Chuo cha Kilimo, mambo ambayo yamewawezesha wakulima kupata mbegu bora na vile vile kuwa na wataalamu wa kutosha kuweza kuwashauri wakulima namna bora zaidi ya kulima na kupata mazao bora yenye tija kubwa.

Kutokana na juhudi hizo, kilimo cha biashara kimeendelea kukua badala ya kile kilimo kilichokuwa kimezeoleka, huduma za afya zimeimarika na huduma za usafiri zimekuwa bora zaidi katika miaka ya hivi karibuni kuliko miaka mingine yote iliyopita. Hali halisi inaonesha kuwa wananchi wengi na hasa vijijini wameanza kuzichangamka fursa hizo na wengi wao wameanza kunufaika.

Hata hivyo, hali bado siyo nzuri kwenye taasisi za umma na mashirika ya Serikali. Kumekuwa na tatizo kubwa la uwajibikaji mionganoni mwa watumishi wa umma. Licha ya Serikali kujaribu kuinua kwa kiasi kikubwa maslahi yao, watumishi wa umma wamekuwa waonekana wakisurasua katika kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Aidha, vitendo vya kukwepa kuwajibika, wizi na ubadhifuru wa mali ya serikali, rushwa, uhujumu wa uchumi na ukiukwaji wa makusudi wa maadili ya uongozi ni mambo ambayo hayanabudi kuchukuliwa hatua zinazofaa. Mambo haya hayana tija katika maendeleo ya nchi yetu

Tuendelee kupoeka misaada ya wafadhili pale tu tunapopewa. Hata hivyo, misaada hiyo kamwe isitufanye kusahau wajibu wetu katika kuleta maendeleo endelevu ya taifa letu. Maendeleo ya nchi huletwala na wananchi wenywewe.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa mgombea Urais wa Zanzibar kwa kipindi cha pili cha Uongozi kupitia CCM akipokea cheti cha Ushindi wa Uchaguzi Mkuu wa marudio kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar Jecha Salim Jecha wakati wa utoaji wa matokeo ya uchaguzi huo yaliyotolewa katika ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja, tarehe 21 Machi, 2016

# Wananchi wa Zanzibar wameamua

## ■ Wamemchagua tena Dk. Shein kuwa Rais

### TUME IMEMTANGAZA, AMEAPISHWA NA AMEUNDA SERIKALI

Tarehe 21 Machi, 2016 imekuwa ni siku nyengine ya kihistoria kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, kwa kushuhudia tukio la Dk. Ali Mohamed Shein kutangazwa tena na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufuatia ushindi mkubwa wa nafasi hiyo aliouposta katika uchaguzi wa marudio uliofanyika Machi 20, 2016.

Licha ya chama kikuu cha upinzani Zanzibar CUF kutoshiriki uchaguzi, idadi kubwa ya Wananchi walijitokeza kupiga kura ilitosha kuthibitisha kuwa wananchi wengi wa Zanzibar bado wamekuwa na imani na kiongozi huyo kuwaongoza kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo. Tume ya uchaguzi Zanzibar ilimtangaza Dk. Ali Mohamed Shein kuwa mshindi kwenye uchaguzi huo kwa kupata asilimia 91.4 ya kura zote halali zilizopigwa. Uchaguzi huo ambaeo ulivishirikisha vyama 14 vya siasa, ulikuwa huru na wa haki.

Kurejewa kwa uchaguzi mkuu wa Zanzibar kunafuatia kufutwa kwa uchaguzi wa awali na matokeo yake



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akionesha cheti cha Ushindi wa Uchaguzi Mkuu wa marudio mara baada ya kutangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, katika ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja, tarehe 21 Machi, 2016



**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na wagombea wa nafasi ya Urais kupitia Chama cha Tadea Bw. Juma Ali Khatib na chama cha ADC Bw. Hamad Rashid baada ya kutangazwa mshindi na kukabidhiwa cheti cha ushindi na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar Jecha Salim Jecha wakati wa utoaji wa matokeo ya uchaguzi mkuu wa marudio yaliyotolewa katika ukumbi wa Salama Bwani Mjini Unguja, tarehe 21 Machi, 2016**

ulofanyika Oktoba 25, 2015 ambao, kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar Bwana Jecha Salim Jecha, alilazimika kuufuta uchaguzi huo na matokeo yake kutohana na kukabiliwa na vikwazo vingi katika kutekeleza majukumu yake aliokabidhiwa kikatiba na kisheria.

Alivitaja baadhi ya vikwazo hivyo kuwa ni pamoja na kutofahamiana kwa wajumbe ndani ya Tume na kufikia hatua ya baadhi yao kuvua mashati na kuanza kupigana, baadhi ya wajumbe badala ya kuwa makamishna wa Tume wamekuwa wawakilishi wa vyama vyao, wakati viro vyama vingi zaidi ambavyo havikupata fursa ya kuwa na makamishna ndani ya Tume hiyo lakini vimeshiriki katika uchaguzi huo. Vile vile kuligundulika kasoro nyingi katika uchaguzi.

Vikwazo vingine ni kufanyika uhamishaji wa visanduku vya kura na kuhesabiwa katika maeneo nje ya vituo kinyume na utaratibu, kutolewa nje ya vituo na kupigwa kwa mawakala wa vyama vingine, hasa wa chama cha TADEA huko Pemba na kuvamiwa kwa vituo na vijana wanaonekana kuandaliwa na vyama vya siasa na kufanya fujo kwa kupiga watu na kuzuia watu wasiokuwa wa vyama vyao kufika katika vituo vya kupiga kura na kupiga kura.

Aidha, Mwenyekiti alivitaja vikwazo vingine kuwa ni pamoja na vyama vya siasa kuonekana kuingilia majukumu ya Tume, ikiwemo kujitangazia ushindi na kupeleka mashinikizo kwa Tume, kuwepo malalamiko mengi kutoka vyama mbali mbali yanayoashiria kutoridhika na mchakato mzima

wa upigaji kura, kuhesabu na kutoa matokeo ya uchaguzi huo. Kadhalika nambari katika fomu za matokeo ya vituo vingi vya Pemba kuonekana kufutwa na kuandikwa upya nambari nyengine juu yake.

Hatua Tume ya Uchaguzi Zanzibar ya kumtangaza Dk. Shein kuwa mshindi na kumkabidhi cheti cha ushindi katika uchaguzi huo, inaashiria mwanzo wa safari nyengine ya kipindi cha pili cha miaka mitano ya uongozi wake wa awamu ya saba wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Akizungumza na wananchi mbali mbali waliohudhuria kwenye hafla ya kutangazwa matokeo, Rais mteule aliahidi kufanyakazi kwa mashirikianona wananchi wote wa Zanzibar bila ya ubaguzi wa aina yoyote kama vile ubaguzi wa kiitikadi, kidini, kijinsia, uzawa au umajimbo.



**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mkewe Mama Mwanamwema Shein wakipongezwa na Mgomea wa Urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo Bw. Khamis Iddi Lila (wa pili kulia) baada ya kutangazwa mshindi wakati wa matokeo ya uchaguzi huo, tarehe 21 Machi, 2016. Picha ya Kulia ni viongozi mbali mbali pamoja na wananchi waliofika kushuhudia tukio hilo katika ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bwani Mjini Unguja**



Rais Mteule wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein akiapishwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Jiji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Omar Othman Makungu katika uwanja wa Amaan Mjini Unguja, tarehe 24 Machi, 2016

#### KUAPISHWA KWA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI



Rais Mteule wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein akipigwa mizinga 21 ikiwa ni salamu za utijfu kutoka kwa majeshi ya ulinzi na usalama mara baada ya kuwasili katika uwanja Amaan Mjini Unguja kwa ajili ya kuapishwa, tarehe 24 Machi, 2016

**M**atokeo ya uchaguzi wa Rais yalifatiwa na sherehe zilizofana za kuapishwa kwa Dk. Shein, ambazo zilifanyika katika uwanja wa Amaan tarehe 24/03/2016 na kuhudhuriwa na maelfu ya wananchi wa Zanzibar kutoka miji na vijiji mbali mbali vya Unguja na Pemba. Aidha Sherehe hizo zilhudhuriwa viongozi wengine

kadhaa kutoka Tanzania Bara, Mabalizi na wawakilishi wa nchi na mashirika mbali mbali ya kimataifa. Miogoni mwa waliohudhuria sherehe hizo ni pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. John Joseph Pombe Magufuli, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Viongozi wastahafu wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama na viongozi wengine kadhaa.

Kiapo cha Mheshimiwa Rais ni kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar kifungu cha 31.(1) kinachoeleza kuwa "Mtu anayechukua madaraka ya Urais, kabla ya kuanza wadhifa huo atakula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kazi kama kitakavyowekwa na Baraza la Wawakilishi lakini kwa hali yoyote itabidi ashike madaraka hayo kabla ya kupita siku saba baada ya kuchaguliwa". Inaelezwa kwenye katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Sherehe za kuapishwa zilikuwa zimepambwa na shamra shamra za kila aina ikiwemo kukagua gwaride la kuapishwa la vikosi vya ulinzi na usalama, mizinga 21 ilipigwa kuashiria kuanza kwa uongozi mpya wa Serikali, ngoma na nyimbo za vijana wa halaiki, tumbuizo za muziki wa taarab asilia na muziki wa kizazi kipyta ilikonga nyoyo za waliohudhuria hafla hiyo muhimu kwa historia ya Zanzibar.

Wakati wa usiku Dk. Shein alijumuika na wana CCM na wananchi wengine wa Zanzibar katika taarab



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwapungia mkuu wananchi baada ya zoezi la kuapishwa pamoja na kukagua gwaride la Vikosi vya Ulinzi na Usalama lenye muundo wa Alfa unaoashiria mwanzo wa Uongozi wake kwa kipindi cha pili cha Serikali ya awamu ya saba katika Uwanja wa Amaan tarehe 24 Machi, 2016

rasmi iliyofanyika katika ukumbi wa Salama Bwawani, ambapo vikundi vitatu vya taarab vilitumbuiza. Vikundi hivyo ambavyo ni mashuhuri kisiwani Unguja ni Kikundi cha Mila na Utamaduni maarufu kama Culture Musical Club, Big Star na Zanzibar Modern Taarab.

Vikundi hivyo vilitia fora na kutoa burudani iliyokonga nyoyo za wageni waalikwa na wananchi wengine waliohudhuria hafla hiyo.

Vikundi vya Culture na Zanzibar Modern Taarab ambavyo vinajumuisha pia wasanii wakongwe katika fani ya muziki huo ‘vilizisuza’ nyoyo za washabiki wa nyimbo za zamani wakati kukundi cha Big Star kilihanikiza washabiki wa Taarab kwa kupiga nyimbo zake kwa mtindo wa kileo zaidi.

Katika Burudani hiyo kila kikundi kilipewa nafasi ya kutumia muda wa dakika 40 ambapo kikundi cha Culture kilifungua pazia kwa kupiga nyimbo ya “mpewa hapokonyeki” ambaa ulilipua vifijo na vigelegele na kuwafanya wapenzi kujimwaga ukumbini kucheza.

Kwa upande wake Zanzibar Modern Taarab vibao vyao “Kupata au kukosa” kilichoimbwa na Rukiya Ramadhani na kingine “Mshayasema Kimeniathiri



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikagua gwaride la Vikosi vya Ulinzi na Usalama lenye muundo wa Alfa katika Uwanja wa Amaan baada ya kuapishwa, tarehe 24 machi, 2016



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipeana mkuu na Kaimu Mkuu wa JKU Kanali Ali Mtumweni Hamadi wakati aliposalimiana na Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama baada ya kumalizika zoezi la kuapishwa katika Uwanja wa Amaan, tarehe 24 machi, 2016



*Mwimbaji wa Kikundi cha Zanzibar One Modern Taarab Bi Rukia Ramadhan akiimba wimbo Natosheka na Ndo ndo ndo katika Taarab rasmi ya kumpungeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa ushindi mkubwa wa kishindo alioupata katika uchaguzi wa marudio, iliyofanyika katika ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bawani Mjini Unguja, tarehe 24 Machi, 2016. Taarab hiyo ilitumbuizwa na Vikundi vya Culture Musical Club, Big Star na Zanzibar One Modern Taarab*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mkewe Mama Mwanamwema Shein, Mkuu wa Mkoja wa Mjini Magharibi Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis, Mama Asha Balozi na Mama Fatma Karume wakifuatilia burudani ya taarab ya kufurahia ushindi wa Dk. Shein katika ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bawani, tarehe 24 Machi, 2016*



*Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein na Mke wa Makamo wa Pili wa Rais Mama Asha Suleiman Iddi wakitunza wakati wa Taarab rasmi ya kumpungeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika ukumbi wa Salama, Hoteli ya Bawani Mjini Unguja, tarehe 24 Machi, 2016*

nini kilichoimbwa na Saada Nassor viliyatia kiwewe washabiki na kuviacha viti vyao.

Kikundi cha Big Star ambacho kinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi, kilionesha umahiri wake kwa kuja na nyimbo zilizouchangamsha ukumbi na kuwafanya wageni na washabiki kukosa kukalia viti vyao muda wote walitumbuiza.

Kibao cha "Hongera Dk. Shein" kilichoimbwa na Tahir Khamis kilinogesha furaha za wana CCM na ikawa hekaheka ukumbini.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria burudani hiyo ni pamoa na wajumbe wa Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM akiwemo Balozi Seif Ali Iddi, Katibu Mkuu wa CCM Abdulrahman Kinana na Naibu Katibu Mkuu CCM Zanzibar Vuai Ali Vuai.

Walikuwepo pia mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwemo Waziri wa Habari, Utamaduni, Michezo na Wasanii Nape Nnauye na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Muungano Januari Makamba.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimuapisha Mhe. Said Hassan Said kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar katika hafla iliyofanyika Ikuu Mjini Zanzibar, tarehe 26 Machi, 2016. Picha nyengine za chini zinaonesha matukio mbali mbali yaliyojitekeza katika hafla hiyo

#### KUTEULIWA MWANASHERIA MKUU NA KUAPISHWA



**K**iongozi wa mwanzo kuanza kuteuliwa na Dk. Shein katika Serikali mpya aliyounda alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Said Hassan Said, ambaye ameteuliwa kuendelea na wadhifa wake huo tarehe 25 Machi, 2016.

Mwanasheria Mkuu ambaye aliapishwa siku iliyofuata tarehe 26 Machi, 2016, ndiyr mshauri wa kisheria wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na atatekeleza shughuli nyengine zozote za kisheria zitakazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Rais au kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984 au sheria nyenginezo zozote.





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimuapisha Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar katika hafla iliyofanyika Ikulu Mjini Zanzibar, tarehe 30 Machi, 2016. Picha nyengine za chini zinaonesha matukio mbali mbali yaliyojitekeza katika hafla hiyo

#### KUTEULIWA KWA MAKAMU WA PILI WA RAIS NA KUAPISHWA



Tarehe 28 Machi, 2016,  
Rais wa Zanzibar na  
Mwenyekiti wa Baraza la  
Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein  
alimteua tena Balozi Seif Ali Iddi kuwa  
Makamo wa Pili Rais na kumuapisha  
tarehe 30 Machi, 2016.

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar  
Makamo wa pili wa Rais atateuliwa  
kutoka mionganini mwa wajumbe wa  
Baraza la Wawakilishi kutoka katika  
chama anachotoka Rais na atakuwa  
ndiye mshauri mkuu wa Rais katika  
kutekeleza kazi zake na pia atakuwa  
ndiye kiongozi wa shughuli za serikali  
katika Baraza la Wawakilishi.

Balozi Seif Ali Iddi ni muwakilishi  
wa kuchaguliwa na wananchi katika  
jimbo la Mahonda, Mkoa wa Kaskazini  
Unguja.





*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikagua gwaride la kikosi cha FFU akiongozwa na Kamanda wa FFU Mjini Magharibi S.S.P Anani wakati wa Uzinduzi wa Baraza la 9 la Baraza la Wawakilishi liliopo Mbweni nje ya Mji wa Zanzibar, tarehe 05 Aprili, 2016*

#### UZINDUZI WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI



**Dk. Ali Mohamed Shein**

*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi*

Tarehe 05 Aprili, 2016, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amelizindua rasmi Baraza la tisa la Wawakilishi. Kabla ya kulihutubia na kulizindua Baraza hilo, Dk. Shein alikagua gwaride la vikosi vya ulinzi na usalama ambalo liliandaliwa maalum kwa ajili ya sherehe hiyo.

Katika hotuba yake kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wote



*Baadhi ya Mabalozi wa nchi mbali mbali wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akitoa hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la 9 iliyofanyika katika ukumbi wa baraza hilo liliopo Mbweni nje ya Mji wa Zanzibar, tarehe 05 Aprili, 2016*

wa Zanzibar, Rais wa Zanzibar alielezea mipango ya Serikali yake katika kipindi cha miaka mitano ijayo huku akisisitiza kutekeleza ahadi zote alizoahidi wakati wa kampeni. Ahadi hizo ni zile zilizomo ndani ya Ilani ya CCM ya mwaka 2015

– 2020 na nyengine nje ya Ilani hiyo. Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuleta mabadiliko ya kiutendaji, kuwjibika katika kazi, kuimarisha uchumi na maendeleo, utawala bora, amani, utulivu na usalama katika nchi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitia saini kitabu cha wageni katika Ofisi ya Baraza la Wawakilishi mara baada ya kuwasili kulizindua Baraza la 9 la Wawakilishi huko kwenye ukumbi wa Baraza hilo Mbweni nje ya Mji wa Zanzibar, tarehe 05 Aprili, 2016. Kulia ni Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid



Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakisikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alipokuwa akitoa hutuba yake ya uzinduzi wa Baraza la 9 uliyofanyika katika ukumbi wa baraza hilo Mbweni, tarehe 05 Aprili, 2016



Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakisimama wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakati alipoingia katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi liliopo Mbweni kabla ya kulizindua tarehe 05 Aprili, 2016



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na wahariri na waandishi wa vyombo vya habari klabla ya kutangaza Baraza la Mawaziri Ikulu Mjini Unguja, tarehe 05 Aprili, 2016

## KUTANGAZWA KWA MAWAZIRI NA MANAIBU MAWAZIRI

Tarehe 9 Machi, 2016,  
Rais wa Zanzibar na  
Mwenyekiti wa Baraza la  
Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein  
alikamilisha uteuzi wa safu ya uongozi  
wa Serikali kwa kutangaza Baraza la  
Mawaziri lenye wizara 13 kutoka 16  
la Awamu ya Kwanza wa Uongozi wa  
Serikali ya Awamu ya Saba. Katika  
Makala haya Mwandishi wetu anaeleza  
zaidi.

Ni tukio lililokuwa likisubiriwa  
kwa hamu na wananchi wote tangu  
kutangazwa matokeo ya uchaguzi tarehe  
21 Machi, 2016 ambapo Dk. Shein  
alibuka mshindi dhidi ya wagombea  
wengine.

Mheshimiwa Rais alitangaza Baraza  
lililo na mchanganyiko wa sura mpya  
na za zamani, wazee kwa vijana na  
kutoa taswira halisi ya mwelekeo wa  
Serikali ya Awamu ya pili ya Uongozi  
wa Awamu ya Saba.

Wamo waliorajiwa na  
wasiotarajiwa pia kama ambavyo  
Mheshimiwa Rais alivyooleza wakati  
akijibu moja ya maswali ya waandishi  
wa habari kuwa si wakati wote uteuzi

wake ungekubaliwa na kila mtu kwa  
kuwa vigezo vya uteuzi ni vingi na  
zaidi uteuzi wa nafasi hizo unazingatia  
pia mahitaji na mweleko wa serikali  
inayoundwa.

Sisi tunaamini kama ambavyo  
Mheshimiwa Rais anavyoamini kuwa  
Baraza hili lina uwezo wa kutekeleza  
malengo ya serikali na kukidhi matarajio  
ya wananchi ambao ndio walengwa  
wakuu.

Jambo kubwa na muhimu  
kwa Baraza hilo na Serikali nzima  
ambalo Mheshimiwa Rais alisisitiza  
ni uwajibikaji usio na mashaka na  
unaozingatia uwazi zaidi.

Masuala haya mawili yamekuwa  
nguzo katika uongozi wa Awamu ya  
Saba chini ya Dk. Shein, ambayo ni  
mionganii mwa ahadi zake zilizogusa  
hisia za wananchi wa Zanzibar katika  
maelezo yake ya kwanza wakati  
alipoleza kwa mara ya kwanza nia yake  
ya kugombea nafasi hiyo mwaka 2010.

Kama alivyooleza wakati wa  
kutangaza Baraza kuwa kipindi cha  
miaka mitano ya kwanza kazi kubwa  
ilifanyika kuweka mazingira bora

yatakayowezesha na kurahisisha  
utendaji na uwajibikaji katika serikali  
kuanzia kwa watumishi wa umma hadi  
viongozi.

"Tumepitisha sheria na kanuni zote  
kilichobaki ni kusimamiwa tu na pia  
tumeweka mazingira ya kuhakikisha  
watu wanafanyakazi na watu  
wanapenda kazi yao" Dk. Shein alisema  
hayo kuwajibu waandishi wa habari.

Lakini kitu ambacho ni wazi na  
Mheshimiwa Rais amekiri kuwa bado  
katika kipindi kilichopita usimamizi  
haukuwa mzuri na suala hilo hata  
baadhi ya wananchi wamekuwa  
wakihoji jambo hilo.

Kwa wote waliokabidhiwa madaraka  
hata kama ni madogo kama vile afisa  
masijala jambo hili si la kufanya  
mchezo. Mathalan haipendezi na ni  
ishara mbaya ikafika wakati wananchi  
kama alivyooleza mwandishi mmoja  
wa habari kuhoji kuwa kama watu  
hawatekelezi maagizo ya Mheshimiwa  
Rais watamsikiliza nani tena.

Ndio maana Mheshimiwa Rais  
alieleza bayana kuwa atawaondoa  
viongozi "wasiosimamia maagizo



ya serikali” na kwamba serikali “itawashughulikia kwa mujibu wa sheria” viongozi na watendaji wasiotekeleza wajibu wao wa kusimamia kazi katika maeneo yao.

Mfano huu wa mifugo mijini, ni kero ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akiisemea mara nydingi lakini uongozi wa Mkoa umekuwa ukisurasua kulitekeleza. Imeelezwa mara kwa mara athari za mifugo kuzurura mjini na hata huko mashamba sehemu za barabarani. Hapa hatua zinapaswa kuchukuliwa.

Katika kusisitiza uwazi Dk. Shein ameahidi kuendelea kuongoza serikali inayozingatia utawala bora na moja ya sifa za utawala bora ni uwazi katika utendaji.

Kwa hivyo alirejea dhamira ya Serikali ya kufanya kazi kwa karibu na vyombo vya habari katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji serikalini na kwamba kila inapowezekana atakutana nao vyombo hivyo kuzungumzia hatua mbalimbali za utendaji wa serikali yake.

“Uwazi zaidi, ukweli zaidi na nyinyi ndio mtakaothibitisha. Mtusaidie kutekeleza kazi yetu hii. Tuwe wakweli

pande zote, tujitahidi kutenda haki, tulipoweza muelege, tulipokosea tuelezwe. Sitawapiga chenga, tutakutana na wizara zitafanya hivyo hivyo” Dk. Shein alisisitiza.

Katika mnasaba huu aliahidi kuziagiza tena wizara na idara za serikali kuweka utaratibu maalum wa kutoa taarifa za Serikali kwa vyombo vya habari ambavyo mara zote amekuwa akitambua nafasi na mchango wake katika kuleta maendeleo ya nchi.

Dk. Shein aliwaeleza waandishi wa habari kuwa hakubaliani na urasimu unaofanywa na baadhi ya watendaji serikalini ambao unakwamisha utendaji wa vyombo vya habari na kuelekeza mamlaka husika kulishughulikia suala hilo mara moja.

Ni jambo la kushangaza kama alivyoeleza mwenyewe Mheshimiwa Rais kuona kuwa watendaji wanakuwa wagumu kutoa habari wakati yeye binafsi anakutana na waandishi mara kwa mara katika shughuli zake za utendaji.

Ni ukweli usiopingika kuwa huo uwazi zaidi wa utendaji wa

serikali ambao Mheshimiwa Rais anaouzungumzia hautaonekana ikiwa kutakuwa na urasimu au hata kutokuwepo ushirikiano na vyombo vya habari.

Changamoto ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa kwa vyombo vya habari kuuelezea umma nini serikali inafanya na wapi imepiga hatua na wapi imerudi nyuma. Kwa maana nyingine hata ule ‘utendaji haki’ alioupigia chapuo Mheshimiwa Rais kwa vyombo vya habari katika kuandika na kuripoti masuala mbalimbali ya serikali hautawezekana kama urasimu hautaondoshwa katika utoaji habari katika serikali na taasisi zake.

Mheshimiwa Rais ameweka wazi vipaumbele vya Serikali katika hotuba yake akizindua Baraza la tisa la Wawakilishi ambapo kama viongozi na watendaji wa serikali hawatazingatia masuala hayo ya uwajibikaji na uwazi itakuwa shida kuvifiki.

Kwa hivyo hadi Baraza la Mapinduzi lilipoapishwa, Viongozi wa serikali, watendaji na hata watumishi wa kawaada walikwishafahamu vyema ujumbe wa Mheshimiwa Rais kwa kuwa wengi wamekuwa wakifuatilia kwa karibu matukio yote hayo kuititia vyombo mbalimbali vya habari.

Kwa hivyo, tunatarajia kushuhudia mabadiliko makubwa katika utendaji wa Baraza la Mapinduzi na Wizara zenye na taasisi za serikali na hatimae wananchi kupata kile wanachokitarajia kutoka kwa serikali yao.

Kama ilivyoeleza awali Baraza la Mapinduzi lina mchanganyiko wa wazoe fu na vijana wenye uwezo hivyo wana kila sababu za kuonesha uwezo wao huo kwa kutekeleza wajibu wao kwa kasi zaidi, ufanisi zaidi na kuongoza kwa mfano wa uwajibikaji kwa wanaowaongoza.

Baada ya kupata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika miaka mitano iliyopita, Mheshimiwa Rais amewahadi wananchi kuwa mambo mazuri bado yanakuja na wa kuyaleta mambo hayo ni sisi sote lakini kiongozi na mtendaji wa serikali ndio muonesha njia. Uongozi ni kuonesha njia. Inawezekana timiza wajibu wako.

## MAWAZIRI WALIOTEULIWA



Mhe. Issa Haji Ussi Gavu  
Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti  
wa Baraza la Mapinduzi



Mhe. Haji Omar Kheri.  
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,  
Tawala za Mikoa na Idara  
Maalum za SMZ



Mhe. Haroun Ali Suleiman  
Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba,  
Sheria Utumishi wa Umma na  
Utarwala Bora



Mhe. Mohammed Aboud Mohammed  
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa  
Rais



Mhe. Dk. Khalid Salum Mohammed  
Waziri wa Fedha na Mipango



Mhe. Balozi Amina Sakum Ali  
Waziri wa Biashara, Viwanda na  
Masoko

## MANAIBU MAWAZIRI



Mhe. Choum Kombo Khamis  
Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na  
Michezo



Mhe. Juma Makungu Juma  
Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na  
Mazingira



Mhe. Khamis Juma Maalim  
Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria,  
Utumishi wa Umma na Utarwala Bora



Mhe. Harusi Said Suleiman  
Naibu Waziri wa Afya



Mhe. Mahmoud Thabit Kombo  
Waziri wa Afya



Mhe. Riziki Pembe Juma  
Waziri wa Elimu na Mafunzo ya  
Amali



Mhe. Salama Aboud Talib  
Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na  
Mazingira



Mhe. Hamad Rashid Mohammed  
Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na  
Uvuvi




Mhe. Moudline Castico  
Waziri wa Kazi, Uwezesajji, Wazee,  
Vijana, Wanawake na Watoto



Mhe. Rashid Ali Juma  
Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na  
Michezo



Mhe. Balozi Ali Karume  
Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na  
Usafirishaji



Mhe. Said Soud Said  
Waziri asiyekua na Wizara Maalum



Mhe. Juma Ali Khatib  
Waziri asiyekua na Wizara Maalum



Mhe. Lulu Msham Abdulla  
Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili,  
Mifugo na Uvuvi



Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri  
Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo  
ya Amali



Mhe. Mohammed Ahmad Salum  
Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na  
Usafirishaji

# Matukio mbali mbali katika **Picha**


Rais wa Zanzibar na  
Mwenyekiti wa Baraza la  
Mapinduzi Dk. Ali Mohamed  
Shein akizungumza na Balozi  
wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania nchini Marekani  
Mhe. Wilson M. Masilingi  
alipofika Ikulu Mjini Zanzibar  
kumsalimia Rais, tarehe 04  
April, 2016



Rais wa Zanzibar na  
Mwenyekiti wa Baraza la  
Mapinduzi Alhaj Dk. Ali  
Mohamed Shein akishiriki  
kusoma Hitma pamoja na  
viongozi wengine na wananchi  
ya kumuombea dua Rais  
wa Kwanza wa Zanzibar  
Marehemu Mzee Abeid  
Amani Karume iliyofanyika  
katika ukumbi wa Ofisi Kuu  
ya CCM Kisiwandui Mjini  
Zanzibar, tarehe 07 Aprili,  
2016

Rais wa Zanzibar na  
Mwenyekiti wa Baraza la  
Mapinduzi Dk. Ali Mohamed  
Shein akizungumza na  
wananchi walioathirika na  
mvua kubwa zilizonyesha  
Jumamosi ya tarehe 16  
April 2016 usiku ambazo  
zilisababisha maafa mbali  
mbali kwa wananchi hao.  
Ziara hiyo ya Rais imefanyika  
tarehe 20 Aprili, 2016





Rais wa Zanzibar na  
Mwenyekiti wa Baraza la  
Mapinduzi Dk. Ali Mohamed  
Shein akizungumza na  
Makamo wa Rais wa Shirika  
la Maendeleo la Korea Kusini  
"KOICA GLOBAL" Bw. Kwon  
Taemyon akiwa na ujumbe  
wake walipofika Ikulu Mjini  
Zanzibar pamoja na mwenyeji  
wa Ujumbe huo Waziri wa  
Kilimo, Maliasili, Mifugo na  
Uvuvi Mhe. Hamad Rashid  
Mohamed(hayupo pichani),  
tarehe 14 Aprili, 2016

Makamo wa Rais wa Jamhuri  
ya Muungano wa Tanzania  
Mama Samia Suluhu Hassan  
na Mke wa Rais wa Zanzibar  
Mama Mwanamwema Shein  
(katikati) Mama Fatma  
Karume (wa pili kulia) pamoja  
na Wake wa Viongozi wakiwa  
katika Hitma ya kumuombea  
dua Rais wa Kwanza wa  
Zanzibar Marehemu Mzee  
Abeid Amani Karume  
iliyofanyika katika ukumbi wa  
Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui  
Mjini Zanzibar, tarehe 07  
April, 2016



Baadhi ya Wananchi  
wa Mjini na Mashamba  
waliojumika kwa  
pamoja katika Hitma  
ya kumuombea dua  
Rais wa Kwanza wa  
Zanzibar Marehemu  
Mzee Abeid Amani  
Karume iliyofanyika  
katika ukumbi wa Ofisi  
Kuu ya CCM Kisiwandui  
Mjini Zanzibar, tarehe  
07 Aprili, 2016



**BAADHI YA DONDODU MUHIMU KAMA ZILIVYOKARIRIWA  
KUTOKA KWENYE HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR  
NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI DK. ALI  
MOHAMED SHEIN KATIKA UZINDUZI WA BARAZA LA TISA LA  
WAWAKILISHI TAREHE 5, APRILI 2016.**

**KAZI ILIYO MBELE YETU**

- Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, katika kipindi chake cha pili itaweka vipaumbele kwa sekta mbali mbali kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 pamoja na ahadi nilizozitoa kwa wananchi, wakati nikiomba ridhaa ya kunichagua pamoja na wagombea wenzangu wa Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu uliomalizika.

**UCHUMI**

- Lengo la Serikali ninayoiongoza, ni kuhakikisha kuwa kasi ya ukuaji wa uchumi inafikia asilimia 8-10 katika miaka mitano ijayo. Shabaha yetu tufikie kiwango cha uchumi wa nchi zenyekipato cha kati, kama ilivyoelekezwa na kusisitizwa katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015-2020, Dira ya Maendeleo 2020 pamoja na mipango mingine ya maendeleo.

Tutahakikisha kwamba tunaimarisha ustawi wa wananchi kwa kuongeza zaidi Pato la Mtu binafsi kutoka kiwango tulichokifikia hivi sasa, cha wastani wa TZS milioni 1.552 sawa na Dola za Kimarekani 939 hadi kufikia kiwango cha Pato la Mtu binafsi kwa nchi zenyekipato cha kati ambacho kinaanza Dola za kimarekani 1,046.

Dhamira ya Serikali katika kipindi hiki cha pili, cha Awamu ya Saba ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka TZS bilioni 362.8 mwaka 2014/2015 hadi kufikia TZS bilioni 800 ifikapo mwaka 2020/2021. Waheshimiwa Wajumbe tuna wajibu na kazi kubwa ya kufanya ili tuweze kuyafikia malengo hayo na Zanzibar iweze kwenda sambamba na kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi nyingi zinazoendelea.

Katika kipindi hiki, tutajitahidi kupanga vipaumbele vichache vinavyotekelzeza kwenye wizara zetu, kwa kutumia uwezo tulio nao na mapato yetu. Tunataka tuanze kujitegemea na hilo ni lazima tuliweze. Nataka Mawaziri na Makatibu Wakuu washirikiane katika kulifanikisha jambo hili. Tutaendelea kupokea misaada kutoka kwa wahisani wetu pale tutakopewa na tutashirikiana nao kwa ajili ya maendeleo yetu.

**UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI**

- Katika kuendeleza juhudi za kuvutia uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uchumi ya Fumba, Serikali imefunga mkataba na Bakhresa Group of Companies ili kujenga miundo mbinu katika eneo ambalo Mpango Mkuu wa Uwekezaji umeshaidhinishwa katika kipindi hiki cha miaka 5. Jumla ya kilomita 13 za barabara kuu zimeanza kujengwa ambazo zitagharimu jumla ya TZS. bilioni 15.6 na barabara ndogo



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitoa hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la 9 la Wawakilishi huko kwenye ukumbi wa Baraza hilo Mbweni nje ya Mji wa Zanzibar, tarehe 05 Aprili, 2016.*

zenye urefu wa kiasi cha kilomita 20 zitajengwa kwa kiwango cha lami zitakazogharimu TZS. bilioni 20.

Jumla ya miradi mikubwa mitano (5) itajengwa kwenye eneo hilo, katika kipindi hiki. Miradi hiyo ni ujenzi wa Miji ya Kisasa wa Kibashara "Fumba Satellite City" katika eneo la Fumba, ujenzi wa Mji wa kisasa wa Makaazi "Fumba Town Development" katika eneo la Nyamanzi, ujenzi wa Mji wa kisasa wa Nyumba za Biashara na Makaazi pamoja na ujenzi wa Maeneo ya Kupumzikia Watu "Fumba Uptown Living" katika eneo la Fumba.

Vile vile, eneo lenye ukubwa wa hekta 102 limetengwa huko Fumba, kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ambapo viwanda viwili vya ujenzi wa nyumba katika vijiji vya Kororo na Nyamanzi tayari vimeshajengwa.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) itaendelea na ujenzi wa nyumba za kisasa uliokwishaanza katika eneo la Mbweni - Unguja, ambao unajumuisha majengo 18 ya ghorofa 7 kila moja. Majengo hayo yatakapomalizika yatakuwa na jumla ya vyumba 252.

## BIASHARA

- Kwa kutambua umuhimu wa zao la karafuu kwa uchumi na historia ya Zanzibar na watu wake, Serikali inaendeleza juhudhi mbali mbali za kuliimarishe zao hili.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, tumepata mafanikio makubwa katika kulifufua zao hilo. Tulianzisha mpango maalum wa miaka 10 wa kulifufua na kuliendeleza zao hili na kwa kulifanyia mageuzi makubwa Shirika la ZSTC ambalo kwa sasa linaendeshwa kwa ufanisi mkubwa.

- Kwa mara nyengine, nawaahidi wananchi kuwa Serikali itaendelea kuwalipa wakulima wa karafuu asilimia 80 ya bei ya karafuu ya soko la dunia kama nilivyoahidi katika kipindi kilichopita. Serikali itaendelea kuwapa mikopo na miche wakulima kutoka kwenye vitalu tulivyovianzisha. Tutaendeleza vita dhidi ya magendo na tutaendelea kuliimarishe Shirika la ZSTC, ili liendelee kusimamia vizuri biashara ya karafuu na viungo vyengine ili lijiendeshe kibashara na liendelee kupata faida. Wito wangu kwa wananchi na wakulima wa karafuu ni kuwa, tushikamane katika kuyaendeleza mafanikio haya. Vile vile, Serikali itaendeleza ujenzi wa barabara za ndani zinazolekeea kwenye maeneo yenye karafuu nyingi. Jumla ya barabara nne zitajengwa kwenye maeneo mbali mbali katika kipindi hiki.

## VIWANDA

- Nataka niwahakikishie wananchi kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, nitasimamia utekelezaji wa ahadi hiyo niliyoitoa wakati wa Kampeni huku tukishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tutazidisha kasi ya kutafuta wawekezaji wenye mitaji mikubwa, uwezo na dhamira ya kweli ya kujenga viwanda katika eneo huru la huko

Micheweni vitakavyokuwa na uwezo mkubwa wa kutoa ajira kwa vijana wetu, kama tulivyokwishaanza kwa eneo la Fumba. Kadhalika, Serikali itaendeleza viwanda katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) na kuwavutia wawakezaji wenye mitaji mikubwa kuwekeza katika miundombinu ya viwanda vinavyotoa ajira kwa wingi.

## UTALII

• Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, tutaongeza kasi ya kuiimarisha sekta ya utalii ili tuweze kulifika lengo lillobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020, la kufikia idadi ya watalii 500,000, wanaoitembelea Zanzibar kwa mwaka, ifikapo mwaka 2020.

Tutaendelea kuwashajiisha wawekezaji ili waje wawekeze katika ujenzi wa hoteli za kisasa na utoaji wa huduma huku tukiwa tumeelekeza nguvu kubwa katika kuimarisha utalii unaozingatia hifadhi ya mazingira na kuulinda utamaduni wetu. Katika kipindi hiki, Chuo cha Utalii cha Maruhubi kitaunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), ili kuimarisha utoaji wa mafunzo ya utalii kwa kutoa shahada za fani mbali mbali. Mafunzo haya yatasaidia katika kuimarisha sekta ya utalii na kuongeza ajira za vijana.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaongeza juhudzi za kuziimarisha sehemu za kihistoria na kufanya matengenezo ya Makumbusho pamoja na kufanya uhifadhi wa mapango ya asili kwa lengo la kuyatunza na kuchochea shughuli za utalii. Kadhalika, Serikali itaendeleza utekelezaji wa Mpango wa Uhifadhi wa Mambo ya Kale na kuanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kale pamoja na vituo vya kuhifadhia kumbukumbu katika kila Mkoa.

## KILIMO

• .....Tutayaendeleza mafanikio pamoja na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoendeleza kuwakabili wakulima wetu. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendeleza kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuendelea kutoa ruzuku ya asilimia 75 ya gharama za pembejeo za kilimo na huduma za matrekta kwa wakulima kama tulivyoanza katika kipindi cha kwanza. Aidha, Serikali itaendeleza programu za mapinduzi ya kilimo na usimamizi wa rasilimali za misitu na kuongeza idadi ya mabwana/mabibi shamba kutoka 172 mwaka 2014 hadi kufikia mmoja kwa kila shehia ifikapo mwaka 2020. Vile vile, tutaendeleza mafunzo kwa wakulima na kutilia mkazo matumizi ya kanuni za kilimo bora katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na matumizi ya zana za kisasa.

Vile vile, Serikali itaendeleza utafiti wa mbegu za mazao ya chakula, biashara, mboga na matunda na kuhakikisha kwamba matumizi ya takwimu na matokeo ya utafiti huo, yanawafikia wakulima na yanatumika katika kufanya uamuzi.

## MIFUGO

• Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendeleza kuhimiza na kuimarisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama, ufugaji wa mbuzi pamoja na kuku wa nyama na mayai, ili kuongeza tija na kipato cha wafugaji.

## UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

• Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendeleza juhudzi katika kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Uvuvi ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari na uhifadhi wa mazingira na kuendeleza jitihada za kuwashamasisha wavuvi wadogo katika kuanzisha vikundi vya ushirika na kuwapatia mafunzo na mikopo nafuu ya zana za kisasa ili kuongeza mapato yao.

Vile vile, Serikali itaandaa mpango na mazingira ya kuvutia Sekta Binafsi kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu, utengenezaji wa boti za uvuvi, ujenzi wa vyumba vya baridi (cold rooms) pamoja na viwanda vya kusindika samaki. Aidha, wavuvi hasa vijana watahamasishwa na kupatiwa mafunzo na zana za kisasa zitakazowawezesha kuvua katika kina kirefu cha maji.

Serikali itanunua vihori 500 vya kuchukulia mwani na kuvisambaza kwa wakulima wa mwani 3,000 Unguja na Pemba ili kuongeza uzalishaji wa mwani. Aidha, itawahamasisha wafugaji wa samaki, chaza, kaa, kamba na majongoo ili kuendeleza uzalishaji wa mazao hayo. Vile vile, juhudzi zitachukuwa katika kutafuta masoko kwa mazao ya baharini. Aidha, tutasimamia Mpango Shirikishi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari yakiwemo maeneo ya Tumbatu, Chumbe – Bawe, Minai kwa Unguja na Kisiwa Panza, Kokota na Mwambe kwa upande wa Pemba. Tutahakikisha kwamba jamii inayozunguka maeneo hayo inanufaika na uhifadhi huo.

Kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaandaa Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na wa nje wawekeze katika Sekta ya Uvuvi wa bahari kuu, wajenge viwanda vya kusindika samaki, waanzishe Chuo cha Mafunzo ya Uvuvi na wajenge Bandari ya Uvuvi. Tayari Kampuni ya Hairu ya Sri Lanka imetiliana saini Makubaliano ya Awali ya kuanzisha uwekezaji katika uvuvi kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile, Serikali imetiliana saini mkataba na Shirika la Kimataifa la Kilimo na Chakula (FAO) kwa ajili ya kuanzisha Mradi wa kuendeleza shughuli za ufugaji wa samaki, utakaogharimu Dola za Kimarekani milioni 3.23. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu na utajumuisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki, huko Beit-el-Ras. Fedha za mradi huo zitatolewa na Serikali ya Korea kupitia Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Kimataifa la Korea ( KOICA).

## **ARDHI**

- Katika kipindi hiki cha pili cha miaka mitano, Serikali itaendelea na juhudzi zake za kuimarishe matumizi ya ardhi na kutatua migogoro iliyobakia na kuimarishe huduma za Mahakama za Ardhi katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Tutaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutambua na kufuata sheria mbali mbali za ardhi zinazohusiana na utambuzi, upimaji na usajili wa ardhi. Aidha, Serikali, itaendeleza kazi ya upimaji wa viwanja na utoaji wa hati kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kiuchumi na kijamii, kwa kuzingatia mpango wa kitaifa wa Matumizi bora ya Ardhi.

## **MAZINGIRA**

- .....Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali italiangalia upya, suala la uchimbaji mawe na mchanga na ukataji ovyo wa minazi. Serikali itaandaa mbinu mpya katika kulishughulikia suala hilo. Nitahakikisha kuwa juhudzi za uhifadhi wa mazingira zinaendelea kupata ufanisi huku tukitambua kuwa dunia imekabiliwa na changamoto mbali mbali zitokanazo na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi. Changamoto hizo zimekuwa na athari zaidi na katika nchi za Visiwa.

## **VYAMA VYA USHIRIKA NA SACCOS**

- Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itayaendeleza mafanikio yaliyopatikana pamoja na kuendelea kuimarishe Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ili kuongeza uwezo wake wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo. Sambamba na juhudzi hizo, Serikali itakiimarisha kituo cha kulelea wajasiriamali kilichoko Mbweni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo mbali mbali kwa lengo la kuwajengea wananchi uwezo wa kujajiri na kuondokana na umasikini.

Aidha, Serikali itaanzisha vituo 10 vya huduma za biashara; kimoja kila Wilaya ili kuongeza tija katika shughuli za wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo pamoja na kutoa mikopo 5,000 yenye thamani ya TZS. bilioni 2.5. Mikopo hii itawanufaisha jumla ya wananchi 50,000 kutoka kwenye makundi mbali mbali ya wananchi hususan wanawake, vijana na watu wenye walemaru.

## **KAZI, AJIRA NA UTUMISHI WA UMMA**

- Suala la ajira bado ni changamoto katika nchi yetu kama ilivyo katika Mataifa mengine. Tuna matumaini makubwa ya kupata mafanikio katika ongezeko la nafasi za kazi katika kipindi kijacho kutokana na mikakati tuliojipangia. Miaka mitano iliyopita, zilipatikana nafasi za ajira 5,370 katika taasisi mbali mbali za serikali na nafasi 25,006 katika sekta binafsi zikijumuisha ajira za nje ya nchi.

Tutahakikisha jitihada za Serikali za kutekeleza mageuzi ya uchumi zinafanikiwa katika sekta ya utalii na viwanda kwa

kuwashajiisha wawekezaji. Tutahakikisha kwamba sekta binafsi inaimarishwa na kuwa chanzo kikuu cha ajira. Vyama vya ushirika navyo vitaunganishwa ili viwawezesha wananchi kubadili maisha yao ili wajiedeleze kiuchumi. SACCOS na Asasi ndogo za fedha zitaimarishwa na kupatiwa mafunzo ya kitaalamu, uongozi na kuwaongezea mitaji, ili ziweze kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi kwa lengo la kuongeza ajira.

Serikali itaendelea na jitihada zake za kuimarishe maslahi ya wafanyakazi pamoja na mazingira ya kufanya kazi. Tutaendelea kuimarishe miundo ya utumishi, ili wafanyakazi waendelee kufaidika na elimu, uwezo na uzoefu walivupata wakiwa kazini pamoja na viwango vya elimu walivyonavyo. Hata hivyo, nataka nikumbushe kuwa, wafanyakazi sote tufahamu kuwa mshahara ni matunda na tunzo mtu anayopata kutokana na juhudzi aliyoifanya katika uzalishaji. Kuna baadhi ya watu wamejenga tabia ya kudai mishahara mikubwa na kuilaumu Serikali kuwa haipandishi mishahara bila ya wao kuwa na ari na dhamira ya kweli ya kujitahidi kufanya kazi na kuzalisha.

....Kwa pamoja tunawajibika kulitekeleza kwa vitendo agizo langu nililolitoa mwaka 2011, mara tu baada ya kuingia madarakani kuwa "tubadilike na tusifanye kazi kwa mazoea". Tulijitahidi kubadilika na kuyaondoa mazoea. Lakini ni ukweli usiopingika matatizo bado yapo, viwango vya utendaji na nidhamu kazini bado havijaongezeka sana. Ni jukumu letu tufanye kazi kwa bidii na tuipende kazi. Kwani wapo baadhi ya wafanyakazi ambao hawapendi kufanyakazi (kwa vitendo vyao), na wengine hawataki kufanyakazi, lakini wao ndio wa mwanzo wanaotaka mishahara mikubwa, posho nzuri, safari za kila wakati na kuhudhuria kwenye semina na mikutano kila mara.

Wapo baadhi ya wafanyakazi kwenye taasisi muhimu zinazotoa huduma kwa wananchi, ambao hawajali kazi zao na wanakwepa wajibu wao. Upo ushahidi kutoka kwa baadhi ya wananchi kwamba wanapokwenda kutaka huduma wanadharauliwa, wanapuuzwa, na wengine wananyanyaswa na wengine hutakiwa watoe kitu chochote. Baadhi ya wafanyakazi wenye tabia hizi walichukuliwa hatua za kinidhamu, lakini bado hawajajirekebisha. Wafanyakazi wa namna hii huwavunja moyo wananchi na hupelekea wananchi waichukie Serikali yao bila ya sababu za msingi.

Zaidi ya hayo, wapo baadhi ya watumishi wenye tabia ya kutoroka kazini, kuchelewa na hawazijali kanuni ziliopo za utumishi wa umma. Wao hujifanya wababe mbele ya viongozi wao. Wafanyakazi wenye sifa mbaya nilizozielezea katika kipindi hiki tutawachukulia hatua watakobainika na kama hapana budi tutawafukuza kazini. Hatuwezi kuwa na wafanyakazi waliokuwa hawana nidhamu. Sasa basi, imetosha. Waliopewa dhamana ya kuziongoza Idara mbali mbali za

Serikali watapaswa watekeleze wajibu wao kwa kuwasimamia wafanyakazi walio chini yao. Pindi kama hawatawajibisha wafanyakazi wao, basi watawajibishwa wao. Lengo letu liwe kutoa huduma kwa wananchi, kwani sote tunawajibika kwao; kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Nataka niwahakikishie wananchi kuwa nitatekeleza ahadi nilizozitoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2015, za kuimarisha maslahi ya wafanyakazi katika sekta mbali mbali ukiwemo utoaji wa kima cha chini cha mshahara cha TZS. 300,000 kwa mwezi ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kuingia madarakani. Kadhalika, ahadi yangu kwa Idara Maalum za SMZ ya maslahi yao yalingane na wenzao wa SMT ipo pale pale. Tumucombe Mwenyezi Mungu atupe uwezo wa kukusanya mapato vizuri, ili Serikali ipate uwezo wa kuzitekeleza ahadi hizo.

## MIUNDOMBINU

- Kwa lengo la kuimarisha zaidi miundombinu ya barabara katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendeleza kazi ya utunzaji na matengenezo ya barabara zilizokwishajengwa na kufanya marekebisho katika maeneo yanayotuama maji ya mvua na kuathiri ubora wa barabara hizo. Kadhalika, tutakamilisha ujenzi wa barabara ya Jendele – Cheju-Kaebona (km 11.7) na barabara ya Koani hadi Jumbi (km 6.3) kwa kiwango cha lami kwa Unguja na barabara ya Ole hadi Kengeja (km 35), Makanyageni hadi Kangani (km 6.5), Finya hadi Kicha (km 8.8) na barabara kutoka Mgagadu hadi Kiwani (km 7.6) kwa kiwango cha lami kwa upande wa Pemba.

Kadhalika, Serikali itajenga jumla ya kilomita 160.8 za barabara kwa kiwango cha lami kwa Unguja katika maeneo mbali mbali ya Mikoa yote na jumla ya kilomita 51.1 kwa kiwango cha lami huko Pemba kwa maeneo yote ya Mikoa ya Pemba. Barabara zote hizi zimefafanuliwa vizuri kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu na mipango yake ya ujenzi tayari imepangwa. Kazi nyengine zitakazoshughulikiwa na Serikali ni kuendeleza kazi ya uwekaji wa taa za kuongozea magari kwa kuweka taa katika sehemu sita, ili kupunguza msongamano katika baadhi ya maeneo ya miji hasa katika mji wa Unguja, Wete na Chake chake.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume (AAKIA), ili kuongeza idadi ya abiria wanaotumia kiwanja hicho pamoja na kiwango cha mizigo ili kuongeza mapato ya Serikali. Kiwanja cha ndege cha Pemba nacho kitapanuliwa ili ziweze kutua ndege kubwa za aina ya Boeing 737, jengo la abiria litajengwa upya na miundombinu na huduma za abiria, ndege na mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba itaimarishwa.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itatekeleza mradi wa ujenzi wa bandari mpya ya kisasa ya kuhudumia mizigo katika eneo la Mpigaduri itakayoanza kujengwa baadae mwaka huu kwa mkopo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Vile vile, bandari ya Malindi itaendelezwu kwa kuongeza vifaa vya huduma kwa abiria pamoja na mizigo. Bandari ya Mkoani Pemba itaendelezwu kwa kuipatia vifaa vya kisasa vya kuhudumia abiria na mizigo. Aidha, bandari ya Wete nayo inatarajiwa kujengwa kwa juhudzi za sekta binafsi, ambapo muwekezaji amejitokeza na yupo tayari kuifanya kazi hiyo. Kadhalika, Gati ya Mkokotoni nayo itajengwa kwa kukamilisha kazi ya ujenzi wa jeti kwa ajili ya huduma za usafiri wa wananchi hasa wa Tumbatu na usafirishaji wa mizigo kwa majahazi.

Shirika la Meli na Uwakala, litafanyiwa mabadiliko makubwa ili liweze kuijendesha kibiashara na kununua meli nyengine mpya ya abiria ndogo na moja ya mafuta.

## NISHATI

- Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendelea na juhudzi za kuufikisha umeme katika vijiji na visiwa vidogo vidogo, vilivybokia ikiwemo Kisiwa cha Fundo, ambapo huduma hizi zinatarajiwa kupatikana katika mwaka wa fedha 2016/2017. Juhudi za kutafuta umeme wa nishati mbadala zimefikia hatua kubwa kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ambapo utafiti wa kutumia upepo unaendelea. Aidha, Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) litafanyiwa mabadiliko, ili liweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na kuijendesha kibiashara.

## UCHIMBAJI WA MAFUTA NAGESI

- Kwa mara nyengine tena, napenda nimpongeze kwa dhati, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuhakikisha kwamba, kabla ya kuondoka kwake madarakani suala la Zanzibar kuchimba mafuta yake wenyewe linapatiwa ufumbuzi. Tulishirikiana kwa dhati katika kulipatia ufumbuzi suala hili. Hivi sasa, Zanzibar ina uwezo wa kisheria wa kuchimba mafuta yake kwa mujibu wa Sheria Namba 21 ya mwaka 2015 iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sina shaka, Baraza hili la Tisa litasimama imara katika kuendeleza pale tulipofika katika kipindi kilichopita na litaharakisha katika utungaji wa sheria tunazozihitaji ili tuweze kuyachimba mafuta na gesi na kufaidika na nishati hizi muhimu.

## HUDUMA ZA JAMII

### ELIMU

- Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itayaendeleza mafanikio hayo katika sekta ya elimu pamoja na kuchukua hatua za kuimarisha elimu katika ngazi mbali mbali. Kuhusu Elimu ya Maandalizi, Serikali itasimamia utekelezaji

wa Sera ya Makuzi na Malezi ya Mtoto na itaanzisha vituo 150 vya Tucheze Tujifunze katika Wilaya nne za Unguja na Pemba.

Kwa upande wa Elimu ya Msingi, Serikali itaongeza kiwango halisi cha uwandikishaji hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2020, itajenga skuli mpya 10 za ghorofa katika maeneo yenye upungufu na msongamano mkubwa wa wanafunzi.

Kadhalika, Serikali itaendelea kulipia gharama za mitihani ya kidatu cha tatu na mitihani ya Taifa kwa watahiniwa wa Kidatu cha Nne na cha Sita. Hatua hii ina lengo la kuwaondolea wazazi mzigo wa kuchangia huduma za elimu ya watoto wao.

Serikali itajenga vituo vipyta vya Mafunzo ya Amali huko Makunduchi kwa Unguja na Daya Mtambwe huko Pemba. Aidha, mafunzo ya ualimu yataimarishwa katika ngazi mbali mbali. Katika kipindi hiki ujenzi wa dakhalia katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) utaanza na ujenzi wa Chuo Kikuu kipyta katika eneo la Dole utaanza kwa kushirikiana na Serikali ya Saudi Arabia. Vile vile, nafasi za masomo ya elimu ya juu zitaongezwa kwa kuuimarisha Mfuko wa Bodi ya Mikopo, ili lengo la kuwanufaisha wanafunzi 22,404 ifikapo mwaka 2020 liweze kufanikiwa.

Katika kipindi kijacho, Serikali itaongeza idadi ya watu wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na kuimarisha Elimu Mjumuisho kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu. Vile vile, Serikali itaimarisha na itaendeleza michezo na utamaduni maskulini ambapo kipindi cha miaka mitano ijayo somo la michezo litaanzishwa katika skuli sita za sekondari zilizoteuliwa. Skuli nne Unguja na mbili huko Pemba.

## AFYA

- Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaongeza jitihada za kuziimarisha huduma za afya kwa kuendelea kuishirikisha sekta binafsi. Azma yetu ya kuifanya hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa itaendeleza kwa kuzikamilisha zile huduma muhimu ambazo bado zinashughulikiwa.

Kadhalika, Serikali itatekeleza mpango wake wa kujenga Hospitali ya kisasa ya Rufaa katika eneo la Binguni Unguja. Ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee unoendelea hivi sasa unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2016. Hospitali ya Wete Pemba nayo itaimarishwa ili hospitali zote mbili zifikiie daraja na kiwango cha Hospitali za Mkao. Aidha, Hospitali ya vijiji ya Makunduchi na Kivunge kwa Unguja zimefika hatua kubwa ya kuwa Hospitali za Wilaya na kazi bado inaendelea kufanywa. Kazi kama hiyo inafanyika kwa hospitali ya Vitongoji na Micheweni.

Serikali vile vile, itakiimarisha Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya kwa kukiunganisha na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, ili kiweze kutoa wataalamu wenye elimu ya kiwango cha shahada katika fani mbali mbali. Kadhalika, madaktari na madaktari mabingwa wa fani mbali mbali watapatiwa mafunzo ili tuweze kujitosheleza na mahitaji yaliyopo. Vile vile, idadi ya madaktari wanaofundishwa katika kitivo cha udaktari katika Chuo Kikuu cha SUZA na vyengine itaongezwa, ili lengo la Serikali lililowekwa kwenye Mpango wa Afya wa mwanzo hapo 1965 wa daktari mmoja ahudumie watu 6,000 liweze kufikiwa. Hivi sasa daktari mmoja anahudumia watu 8,885 (1:8885).

Vile vile, tafti mbali mbali katika maeneo ya Afya ya mama na mtoto, maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza zitaendelezwa pamoja na mifumo ya utoaji huduma za afya. Huduma za matibabu ya wagonjwa walioathirika na dawa za kulevyta na afya ya akili zitaimarishwa na kujenga kituo maalumu kwa waathirika wa dawa za kulevyta. Serikali itaongeza bidii katika kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevyta ili kuwanusuru vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa. Aidha, Serikali itaimarisha upatikanaji, ugawaji, usambazaji na udhibiti wa dawa, vifaa vya utibabu, dawa za uchunguzi wa maradhi na “reagents” zenye ubora. Vile vile, Serikali itaandaa Sheria ya Uanzishaji wa Mfuko wa Bima ya Afya na kusimamia utekelezaji wa mfuko huo. Kadhalika, Serikali itaandaa utaratibu mzuri wa namna wananchi watakavyochangia huduma za afya wanapoeleza kufanya hivyo. Hivi sasa hakuna mpango unaofahamika katika jambo hili.

## MAJI

- Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaendelea kuimarisha usambazaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi kutoka asilimia 87 mwaka 2015 hadi asilimia 97 mwaka 2020 kwa mijini na kutoka asilimia 70 mwaka 2015 hadi asilimia 85 kwa vijiji ifikapo mwaka 2020. Vile vile, itaendeleza jitihada za kuimarisha miundombinu ya maji ili kupunguza upotevu wa maji. Vyanzo vya maji vitahifadhiwa, vitatunzwa na vitalindwa pamoja na maeneo ya kuhifadhia maji. Vile vile, wananchi watahamasishwa juu ya umuhimu wa uhifadhi, utumiaji na uchangiaji wa huduma ya maji safi na salama. Utafiti wa matumizi ya nishati ya juu katika visima na vyanzo vya maji utafanywa, kwa lengo la kapatikana huduma hizi kwa ufanisi.

## VYOMBO VYA HABARI

- Katika kipindi cha miaka 5 ijayo, Serikali itahakikisha kwamba uhuru wa vyombo vya habari unaendelea kuimarishwa na vyombo hivyo vinatimiza wajibu wake kwa weledi na kuzingatia maadili ya kazi zao. Serikali itaimarisha matumizi ya TEHAMA na kuendeleza mageuzi ya sekta ya Habari, ili kuongeza ufanisi na weledi.

Vilevile, Shirikala Habari la Zanzibar (ZBC) litaimarishwa kwa kulipatia mitambo, vifaa nya kisasa ili kuukamilisha utaratibu wa matumizi ya "Digital" kwa TV na Redio. Aidha, mafunzo ya wafanyakazi wake katika kada mbali mbali yataolewa ndani na nje ya nchi. Tutaendelea kuwashajihisha wawekezaji ili wawekeze katika vyombo nya habari binafsi.

Kuhusu Kiwanda cha Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Serikali itakiimarishe na kukiongezea vifaa na wataalamu. Vile vile, Serikali itakiimarishe Chuo cha Uandishi wa Habari ili kiwe chachu ya kuendeleza tasnia ya habari na kuendeleza vipaji nya uandishi wa habari.

Hata hivyo, tasnia ya habari imekabiliwa na changamoto ya matumizi mabaya ya intaneti na mitandao ya kijamii. Matarajio yangu ni kuwa wakati utakapofika mtahakikisha mnajadili na mnairidhia Sheria ya Makosa ya Matumizi ya Mitandao ya Mwaka 2015 iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili sheria hii iweze kutumika hapa Zanzibar. Lengo letu tuwe na matumizi ya mitandao yanayozingatia sheria, heshima, faragha na haki za wananchi pamoja na utunzaji wa siri za Serikali.

## UTAMADUNI NA MICHEZO

- Katika kipindi hiki cha pili, Serikali itaendelea na juhudzi za kuulinda, kuudumisha na kuutangaza utamaduni wa Mzanzibari kwa kuendelea kuandaa matamasha ya utamaduni. Aidha, tutawaelimisha wananchi hasa vijana juu ya matumizi bora ya mitandao pamoja na kufanya ukaguzi wa kazi za sanaa mbali mbali. Tutaendelea na jitihada za kuimarishe lugha ya Kiswahili na kuzifanya lajaja za Zanzibar kuwa ni chimbuko la Kiswahili fasaha. Vile vile, tutaendelea kuimarishe tasnia ya sanaa kwa kuongeza kasi ya kutafuta na kukuza vipaji nya wasanii pamoja na kuimarishe maslahi yao kwa kuimarishe mfumo uliopo wa matumizi ya hakimiliki.

Vile vile, tutazidisha juhudzi zetu katika kuyaendeleza mafanikio tuliyoyapata katika sekta ya michezo kwa kuyaimarishe mashindano ya riadha ya Wilaya na kuliimarishe Bonanza la michezo la vikundi nya mazoezi. Jitihada zetu za kuimarishe michezo katika maskuli, bila ya shaka zitafanikiwa. Kadhalika, tutakamilisha matengenezo ya Kiwanja cha Mao Tse Tung na kujenga viwanja nya michezo kwa kila Wilaya. Tutahamasisha ushiriki wa michezo na ufanyaji wa mazoezi ya viungo kama ni hatua muhimu ya kuimarishe afya za wananchi. Tutaendelea michezo ya asili ya Zanzibar, ikiwemo mashindano ya resi za ngalawa, bao, karata, michezo wa ng'ombe na mengineyo.

Watu wenye ulemavu nao tutawahamasisha kwa kuwapatia vifaa pamoja na vyama nya michezo vinavyohusika, ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuendeleza michezo. Wasanii wataendelea kusaidiwa, wataendelezwa na wale waliojenega nchi yetu heshima katika ulimwengu wa utamaduni, wataenziwa na watapewa heshima yao.

## KUYAENDELEZA MAKUNDI MAALUM

### VIJANA

- Kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili vijana, Serikali katika kipindi kijacho cha miaka mitano, itachukua hatua za kuuimarishe mfuko maalum wa vijana, ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika na mfuko huo na kwenye kazi mbali mbali pamoja na kujajiri katika kilimo cha kisasa na kuanzisha "green house" moja kwa kila Wilaya. Aidha, Serikali itawahamasisha vijana 5,000 waliomiliza vyuo Vikuu kuanzisha vikundi nya uzalishajimali na utoaji wa huduma na kuwapatia mafunzo na mikopo ili waweze kujajiri. Kadhalika, Baraza la Vijana litaendelezwa, ili kuongeza ushiriki wa vijana katika ngazi mbali mbali za uamuvi. Aidha, jitihada za Serikali za kuongeza ajira kwa kushirikiana na sekta binafsi, zitaendelezwa.

### WANAWAKE

- Kwa lengo la kuwawezesha wanawake kiuchumi, kijamii na kisasa katika miaka mitano ijayo, Serikali itayaendeleza yale mafanikio yote yaliyopatikana. Vile vile, itaendelea kusimamia upatikanaji wa haki za wanawake na kupiga vita mila na desturi zinazowabagua au kuwadhalilisha na kusimamia utekelezaji wa sheria na mikataba yote ya Kimataifa inayohusu ustawi wa wanawake. Aidha, Serikali itaanizisha jumla ya vikundi 500 nya wanawake na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali pamoja na mikopo ili waweze kujajiri wenye. Kadhalika, kituo kiliopo Kibokwa cha kuwafundisha wanawake kutengeneza vifaa nya umeme wa jua kitaendelea kuimarishe ili kiwafundishe wanawake wengi zaidi. Vile vile, kampeni ya kupinga udhalilishaji wanawake na watoto itaendelezwa kwa kasi, ili hatimae matatizo haya yasiwepo kwenye jamii zetu.

### WAZEE

- Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaongeza juhudzi katika kuimarishe huduma za kijamii na mahitaji muhimu wanayopewa wazee wanaotunzwa katika nyumba za wazee za Unguja na Pemba. Kadhalika, Serikali itaanza kutekeleza Mpango wa kuwapatia Pencheni maalum wazee wote waliofikia umri wa miaka 70 bila ya kujali historia ya kazi walizokuwa wakizifanya. Vile vile, Serikali itaandaa utaratibu maalum wa kuwapatia wazee huduma za matibabu bure.

### WATOTO

- Ili kuhakikisha haki za watoto zinaendelea kulindwa, katika kipindi kijacho Serikali itayaendeleza yale mafanikio yote yaliyopatikana. Vile vile, itaziimarishe Mahkama za watoto na kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa mabaraza ya watoto na kamati za wazazi katika Shehia, Wilaya na Mikoa yote ya Zanzibar, ili kupinga vitendo nya udhalilishaji dhidi ya watoto. Kadhalika, jitihada zetu za kupiga vita ajira za watoto zitaendelezwa pamoja na kusimamia utekelezaji wa sheria na mikataba ya Kimataifa inayohusu haki, usawa na hifadhi ya mtoto.

## **WATU WENYE ULEMAVU**

• Watu wenye ulemavu wana haki kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984, kutambuliwa utu wao, kuendelezwa, kuheshimiwa, kushirikishwa na kulindwa dhidi ya vitendo vinavyowabagua. Katika kipindi hiki, tutaendeleza kusimamia utekelezaji wa mipango na programu mbali mbali zenye lengo la kuwaendeleza watu wenye ulemavu. Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu tuliuanzisha kipindi kilichopita utaimarishwa na tutahakikisha kuwa huduma muhimu na mahitaji ya nyenzo zote pamoja na dawa zinapatikana bila ya malipo. Aidha, tutaendeleza na utoaji wa mafunzo na elimu kwa wazazi, walezi na walimu juu ya namna ya kuwakuza watoto wenye ulemavu na tutayazingatia makaazi yao wanayoishi.

## **DEMOKRASIA NA UTAWALA BORA**

• Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itaongeza kasi katika kuziendeleza juhudhi za Demokrasia na utawala bora kwa lengo la kuongeza ufanisi. Pamoja na mambo mengine, Serikali ina mpango wa kujenga jengo jipya la Mahkama Kuu huko Tunguu, kukamilisha ujenzi wa Mahkama ya Watoto Mahonda na kuyafanya matengenezo makubwa majengo ya mahkama ya Mfenesini, Mwanakwerekwe na Wete na kuzisogeza huduma za Mahkama karibu na wananchi.

Katika kusimamia maadili ya viongozi na nidhamu ya utumishi, Serikali katika kipindi kilichopita ilianzisha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Namba 1 ya 2012 na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2015. Kufuatia sheria hiyo, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na hivi karibuni nitaianzisha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Katika kipindi hiki, nitahakikisha kwamba Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, inafanya kazi ipasavyo ili viongozi wote waliotajwa katika sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma wanatangaza mali zao kwa mujibu wa sheria hio. Kila kiongozi atatakiwa atekelze wajibu wake kwa wakati uliowekwa. Katika kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi, Serikali haitomvumilia mtu ye yeyote atakayebainika kuzibeza na kutaka kuzirudisha nyuma jitihada za Serikali kuto kana na udhaifu wake wa kimaadili.

Hapana asiyejua kuwa rushwa ni adui wa haki na Mwenyezi Mungu ameikataza rushwa. Katika kulikemea jambo hili, Mwenyezi Mungu katika aya ya 188 ya Surat Al-Baqarah ametuasa kwa kusema: "Wala msiliane mali zenu kwa batili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua". Kadhalika, ipo hadithi mashuhuri ambapo, Mtume Muhammad (SAW) amesema kwamba: "Mwenyezi Mungu amemlaani mtoe rushwa na mpokeaji rushwa na anaeshuhudia na anaeandika".

Lakini Serikali nayo inaichukia na inaipiga vita, ndio maana tunafanya jitihada za kushughulika nayo na tumelazimika kutunga Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kwa upande mwengine, wananchi nao wanaichukia rushwa na hawavipendi vitendo vinavyoambatana nayo. Wapo wananchi wanaovijua vitendo vinavyoashiria rushwa ambavyo vinafanya katika maofisi yetu, inasemekana baadhi yao wanadiriki kuvisema. Tutawachunguza viongozi na watumishi wanaofanya vitendo hivyo, kwa kuzingatia sheria na taasisi zake, ili tuujue ukweli na hatimae tuchukue hatua. Iwapo mambo hayo yanayofanyika, wanayoyasema baadhi ya wananchi; ndio hayo yanayoitwa majipu, basi nataka niahidi, tutayatumbua na moyo wake tutautoa.

Nataka niwahakikishie wananchi kwamba, kauli yangu hii si maneno matupu bali yataambatana na vitendo.

Vile vile, katika jitihada zetu za kusimamia matumizi bora ya fedha za umma, Serikali itadhibiti na kuzuwa safari za nje za kikazi zisizo za lazima. Semina, kongamano na mikutano inayofanya kwa kutoa posho wakati wa saa za kazi, itawekewa utaratibu mpya. Serikali itahakikisha kuwa ubora wa miradi inayotekelza na ununuzi wa vifaa na huduma mbali mbali zinalingana na thamani ya fedha zilizotumika (Value for Money). Zipo taarifa kwamba kuna ubabaishaji mkubwa unafanyika, katika ununuzi wa vifaa na nyenzo. Ni jukumu la Watendaji Wakuu na wale wote wenye dhamana ya manunuzi na kuidhinisha miradi, kuzingatia Sheria Namba 9 ya 2005 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, wahakikishe kwamba taratibu zote za manunuzi zinafuatwa.

Nachukua nafasi hii, kuwahimiza viongozi watakaopewa nyadhifa mbali mbali kuwa wabunifu katika kupanga na kutekeleza mipango iliyo kwenye dhamana walizokabidhiwa. Ni vigumu kwenda katika kasi tunayoitaka ikiwa kila kiongozi atategemea maelekezo na mipango kutoka kwa Rais au Makamu wake ndipo atekelze wajibu wake. Nawahimiza viongozi watakaopewa dhamana kutumia utaalamu wao kwa kuleta maendeleo na lazima wailewe mipango na sheria zinazohusiana na majukumu waliyopewa na taasisi wanazozifanyia kazi na kuzitekeleza ipasavyo. Lazima waifanye kazi ya kuwasimamia watumishi walio chini yao na wale watakaozikiuka sheria na taratibu watapaswa wawachukulie hatua na kuwawajibisha. Kama hawatafanya hivyo, basi na wao watawajibishwa.

Katika utekelezaji wa utawala bora, nitaendelea kuhakikisha kuwa Mihimili yetu Mitatu, (Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahkama), kila mmoja unafanya kazi ukiwa huru na kwa mujibu wa sheria zilizobainishwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Tutahakikisha kila muhimili unapata fedha za kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa uwezo wa Bajeti ya Serikali na si zaidi ya hilo. Hapatakuwa na fedha za ziada, zaidi ya zile zitakazopitishwa katika bajeti.

## IDARA MAALUM ZA SMZ

• Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali itazidi kuziimarisha Idara Maalum za SMZ kwa kuwapatia watendaji wake mafunzo, vifaa vya kisasa na kuimarisha maslahi yao kadri hali itakavyoruhusu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Nitatekeleza ahadi yangu niliyoitoa kwao wakati wa Kampeni za uchaguzi ya kuangalia upya maslahi yao ili yalingane na wenzao wa SMT kwa lengo la kuwapunguzia ukali wa maisha na kuongeza ufanisi katika kazi zao. Kama nilivyooleza hapo mwanzo kwamba, suala hili litategemea uwezo wa Serikali katika kukusanya mapato. Uamuzi si tatizo na tayari nishaufanya.

## USHIRIKIANO NA NCHI NYENGINE NA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE

• Katika uongozi wangu, nitahakikisha Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaendelea kuwa na uhusiano na mashirikiano mema na nchi mbali mbali duniani pamoja na Mashirika ya Kimataifa juu ya masuala mbali mbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha ushirikiano na Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya nyengine za Kikanda ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama.

Katika kipindi cha pili cha Awamu ya Saba, nitahakikisha tunazidi kukiimarisha Kitengo maalum nilichokianzisha cha kuratibu masuala ya Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje ili kiendelee kuwashajiisha kushiriki katika shughuli za maendeleo ya nchi yetu.

Napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa "Wanadiaspura" kwa michango mikubwa wanayoendelea kuitoa, ya hali na mali, kwa ajili ya kuendeleza sekta za kiuchumi na kijamii hasa kuendeleza elimu, afya, biashara na uwekezaji. Nawaomba waendelee kuwa pamoja nasi kwani; 'Mtu Kwao ndio Ngao'.

## KUWAUNGANISHA WANANCHI WA ZANZIBAR

• ..... .Sote tunafahamu kwamba tarehe 20 Machi, 2016, tulikuwa na Uchaguzi Mkuu wa marudio ulioendeshwa na kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984 na Sheria ya Uchaguzi Nambari 11 ya mwaka 1984. Madhumuni ya uchaguzi huo yalikuwa ni kuchaguliwa kwa viongozi wa vyama vya siasa wakataoingoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Katika Uchaguzi Mkuu huo wa Marudio wa tarehe 20 Machi, 2016 nafasi ya Rais iligombewa na vyama 14 vya siasa na hakukuwa na Chama chochote zaidi ya Chama cha Mapinduzi, kilichopata matokeo ya kura za Uchaguzi wa Rais kwa zaidi ya asilimia 10. Mimi nikiwa Mgombea wa Urais wa CCM, nilipata asilimia 91.4. Kadhalika, hakukuwa na Chama

cha siasa zaidi ya CCM chenye wingi wa Viti vya Majimbo katika Baraza la Wawakilishi. Kwa kuzingatia msingi huo, na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 39(3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, hakuna Chama cha siasa ambacho kinakidhi masharti ya kustahiki kutoa Makamo wa Kwanza wa Rais ili kuunda Serikali ya Umoja wa Kitifa. Huo ni uamuzi wa wananchi wa kukipa ushindi mkubwa Chama cha Mapinduzi na hawakutoa nafasi ya kumchagua Makamu wa Kwanza wa Rais. Huo ni uamuzi wao wa kidemokrasia. Kadhalika, uteuzi wa nafasi ya Makamo wa Pili wa Rais umewekewa masharti na kifungu cha 39(6), kuwa:-

- (i) Atateuliwa kutoka mionganoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.
- (ii) Atoke katika chama anachotoka Rais. Uteuzi nilioufanya wa kumteua Makamu wa Pili wa Rais umekidhi matakwa ya kifungu cha 39(6) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Nimelazimika nilieleze jambo hili la kikatiba, kwa sababu wapo waliodhani kuwa yupo Mgombea anayestahiki kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini Rais amekataa kumteua na hivyo Katiba imekiukwa. Nililolifanya, la kumteua Balozi Seif Ali Iddi kuwa Makamo wa Pili wa Rais ni sahihi na ni kwa mujibu wa Katiba na nimechukua hatua ya kuunda Serikali kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwamba Serikali nitakayoiunda itasimamia misingi ya haki, uwajibikaji, uwazi na usawa kwa wananchi wote, bil ya kumbagua mtu ye yeyote kutokana na itikadi yake, dini yake, jinsia au eneo analotoka. Mimi ni Rais wa wananchi wote wa Zanzibar. Nitashirikiana na viongozi mbali mbali, wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, na kadhalika. Zanzibar ni yetu sote, viongozi wa vyama vya siasa tuna jukumu la kushikamana na kuwatumikia wananchi kwa ajili ya maendeleo yao.

Nataka nirudie ule usemi wangu wa mwanzo kwamba, viongozi jukumu letu hivi sasa, kila mmoja wetu na sote kwa pamoja tufanye kazi kwa bidii na maarifa tupate maendeleo tunayoyakusudia. Uchaguzi umekwisha na washindi wamepatikana [ndio sisi tuliomo humu ndani na wengine nitawachagua] ili tuiongoze nchi yetu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, hadi hapo utakapofanyika uchaguzi mwengine mwaka 2020. Hakuna uchaguzi Mkuu mwengine.

## KUIMARISHA MUUNGANO

• Suala la kulinda na kudumisha Muungano wetu wa Serikali mbili, kwangu halina mbadala. Nitaendelea na juhudhi za kudumisha Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar wa Serikali mbili, ulioasisiwa mwaka 1964 ambaa unatimiza Miaka 52 ifikapo tarehe 26 Aprili 2016.



## MAONI YA WANANCHI KUHUSIANA NA USHINDI MKUBWA WA DK. SHEIN KWENYE UCHAGUZI MKUU WA TAREHE 20 MACHI, 2016

Kumekuwa na mijadala tofauti inayoendelea kuhusiana na uamuzi wa kidemokrasia wa wananchi wa Zanzibar wa kumrejesha tena madarakani Dk. Ali Mohamed Shein kuiongoza Zanzibar kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Mijadala hiyo imekuwa ikijikita zaidi kwenye tathmini ya utekelezaji wa masuala mbali mbali katika kipindi kilichopita cha uaongozi wake, ikiwemo utekelezaji wa ahadi alizozitoa, hali ya uchumi, siasa na huduma za jamii nchini. Wachache wamezungumzia kitendo cha Chama cha upinzani cha kususia uchaguzi huo kutokana na kitendo hicho kutokuwa na athari yoyote kwenye uchaguzi huo.

Hata hivyo, siasa katika kipindi chote cha uchaguzi na hata kabla na baada ya kipindi hicho, imeonekana kuwa ni suala nyeti linalogusa nyoyo za watu wengi wa Zanzibar na ni wazi kwamba suala hili linahitaji umahiri na tahadhari ya aina yake katika kulishughulikia.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Zanzibar imepiga hatua kubwa ya kupigwa mfano kisiasa. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa ilikuwa ni ya kwanza ya aina yake Afrika, na iliundwa wakati Zanzibar ikitokea kwenye uhasama mkubwa wa kisiasa baina ya vyama viwili vikuu vinavyopingana kwa sera na mwelekeo.

Wengi walitarajia kwamba muundo huo wa serikali kwa vyovyyote vile usingeweza kudumu kwa zaidi ya mwaka mmoja kutohana na uzoefu, hulka, sera na tabia za baadhi ya viongozi ndani ya vyama vinavyounda serikali hiyo.

Pamoja na dhana hiyo waliyokuwa nayo baadhi ya watu wa Zanzibar, Tanzania na hata nje ya Tanzania, kwa ujumla watu walishuhudia miaka mitano ya serikali hiyo ikimalizika kwa amani na maelewano, ingawa kulikuwa na changamoto nyingi za kisiasa ndani ya kipindi hicho.

Mara kadhaa Rais wa Zanzibar na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikaririwa na vyombo vya habari kutoka kwenye mazungumzo yake na wananchi akisema kuwa "...ni vigumu kuamini kwamba kwenye Baraza la Mapinduzi kuna Mawaziri kutoka vyama viwili vya CCM na CUF wakati Baraza hilo linapojadili masuala yene maslahi na Zanzibar. Sote tunakuwa kitu kimoja tunajadili masuala ya nchi yetu tukitekeleza Ilani ya CCM 2010 – 2015; kama isingekuwa kukwazwa na taratibu za kisheria, natamani sana nikualikeni siku moja mje kushuhudia" alisema Dk. Shein kwenye mmoja ya mikutano yake na wananchi Pemba.

Kilichomuwezesha Dk. Shein kufanikiwa vyema kisiasa kwenye awamu hiyo ni upeo wake mkubwa katika kuifahamu demokrasia, kuheshimu katiba na utawala wa sheria. Katika utawala wa demokrasia suala la uvumilivu wa kisiasa linachukuwa nafasi ya pekee, na uzoefu unaonesha kuwa viongozi wengi wa kisiasa wanashindwa katika jambu hilo.

Lakini suala jengine muhimu alilolizingatia Dk. Shein ni uhuru wa mtu kutoa maoni yake kama liliyoelezwa katika katiba zote mbili za Tanzania – Katiba ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Inasemekana kwamba sifa hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa katika ushindi wa kishindo, aliouputa Dk. Ali Mohamed Shein kwenye uchaguzi Mkuu wa Machi 20, 2016.

Uongozi wa Dk. Shein katika kilipindi cha miaka mitano iliyopita vile vile umeleta mafanikio makubwa ya kiuchumi Zanzibar. Serikali imepiga hatua ya kupigiwa mfano katika kujenga misingi imara ya uchumi ndani ya kipindi cha miaka mitano iliyopita. Katika kipindi hicho cha miaka mitano ya kwanza, uchumi wa Zanzibar ulikuwa kwa asilimia 6.6, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa tokea kuanza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Bila ya shaka kasi hiyo ya ukuaji wa pato la taifa ilichangiwa zaidi kutokana na kuimarike kwa sekta ya huduma na sekta ya viwanda, kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini pamoja na kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu.

Vile vile wananchi wengi wanazungumzia kwa matumaini makubwa juu ya jitihada zilizofanyika kuinua pato la taifa ambalo liliweza kuongezeka kutoka TZS bilioni 1,050.8 mwaka 2010 hadi kufikia TZS bilioni 2,133.5 mwaka 2014 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 103.

Mafanikio hayo sambamba na ongezeko la pato la mtu binafsi ambalo nalo limeongezeka kutoka TZS 856,000 sawa na Dola za Kimarekani 613 mwaka 2010 hadi kufikia TZS milioni 1,552 sawa na Dola za Kimarekani 939 mwaka 2014, yalimpa sifa ya ziada Dk. Ali Mohamed Shein kuweza kuchaguliwa kwa kishindo kuiongoza tena Zanzibar, tofauti na wagombea wengine walioshiriki kwenye uchaguzi huo.

Kuhusu huduma za jamii, pamoja na wananchi wengi kuonesha kuridhishwa na jitihada mbali mbali za serikali katika kuimarisha huduma za elimu, afya



maji safi na salama, wananchi wengi wameonekana kufurahishwa zaidi na uamuvi wa Rais wa kuamua kuondoa michango yote iliyokuwa ikitolewa na wazazi katika elimu ya msingi, na kwamba wanaburiri kwa hamu kuona ufanisi katika utekelezaji wa dhamira ya serikali ya kuendelea kulipia gharama za mitihani ya kidato cha tatu na mitihani ya taifa kwa watahiniwa wa kidato cha nne na cha sita.

Malalamiko yaliyoonesha wananchi kukerwa na vile vile kuchoshwa na vitendo vya udhalilishwaji wa kijinsia, rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, yamekuwa yakisikika katika maskani, baraza na vijiwe kadhaa kabla ya uchaguzi mkuu. Wananchi wengi walionekana kufurahia kauli za Dk. Shein kwenye mikutano yake mbali mbali alipokuwa akijibu masuali

aliyochomekewa na wananchi kila walipopata nafasi ya kufanya hivyo, kwa kuahidi kuwa baada ya uchaguzi mkuu atakapoingia madarakani atatumbia majipu na mioyo yake.

Majibu ya masuali hayo nayo yaliwapa matumaini makubwa wananchi wapiga kura, wakifarajika na hatua za Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Dk. John Pombe Magufuli, mgombea wa CCM ambaye anaendelea kujizolea sifa kutokana na hatua mbali mbali za kupambana na ujisadi, ambazo amekuwa akizichukua mara tu baada ya kushika ofisi.

Aidha, wananchi wameonesha kutiwa moyo kwa kumuona Dk. Ali Mohamed Shein yuko mstari wa mbele katika harakati mbali mbali zinazolenga kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia



**Baadhi ya wananchi waliohudhuria sherehe za kuapishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakisikiliza kwa makini hotuba yake kabla ya wao kutoa maoni yao kuhusu ushindi wa Dk. Shein katika uchaguzi mkuu wa marudio iliofanyika tarehe 20 Machi, 2016**

pamoja na kulizungumzia kwa uchungu  
mkubwa suala hilo kila anapopata fursa  
ya kufanya hivyo.

Kwa kuwa hatua hiyo ni utekelezaji  
wa Ilani ya CCM, wapiga kura wengi  
walipata matumaini zaidi kwa Dk. Shein  
na hivyo kuzidi kummiminia kura.

Suala gumu ambalo linaendelea  
kuwasumbua wananchi wengi na  
kuliona kuwa ni changamoto kubwa  
kwa serikali, ni namna itakavyoweza  
kukabiliana na wahalifu wa makosa  
mbali mbali hasa makosa ya jinai  
ikiwemo kesi za udhalilishaji.

Ugumu wa suala hilo umeonekana  
pale ambapo baadhi ya watu  
wanaonekana wazi kuwa wanavunja  
sheria za nchi, wanahatarisha amani  
ya nchi ambayo ndiyo pekee yenye  
kuwapa watu kuishi kwa matumaini,  
watoto wanaharibiwa lakini wahusika

wanaachwa bila ya kuchukuliwa hatua  
za kisheria. Kinyume chake, watoto  
wa wanyonge ambao hufanya makosa  
madogo k.m kuiba ndizi, kuku, nazi  
au bidhaa za vyakula mashambani,  
hufikishwa kwenye vyombo vyya sheria  
na kuhukumiwa kifungo cha muda  
mrefu jela.

Wapo wengine wenye kufanya  
makosa madogo ya kibinadamu kwenye  
sehemu zao za kazi na kuchukuliwa  
hatua kali za kinidhamu, lakini wapo  
wenye kufanya makosa makubwa na  
kuisababishia serikali hasara kubwa.  
Kwa bahati mbaya watu wa aina hiyo  
huachwa bila ya kuchukuliwa hatua  
zozote za kinidhamu.

Ni matumaini ya wengi kwamba,  
awamu ya pili ya Serikali chini ya  
uongozi wa Dk. Shein itaimarisha  
zaidi utawala wa sheria kwa kuzingatia

kwamba binadamu wote ni sawa  
mbele ya sheria, na wote wanayo haki,  
bila ya ubaguzi wowote, kulindwa  
na kupata haki sawa mbele ya sheria.  
Ni wazi changamoto hizi zinabaki  
kwenye vyombo vyya sheria na mamlaka  
zinazosimamia sheria na kanuni za  
utumishi wa umma ikiwemo tume ya  
maadili itakayoundwa baadee.

Hili ni kwa upande mmoja,  
lakini kwa upande mwengine taasisi  
zinazoshughulikia masuala ya sheria  
nazo hazina budi kuendelea kutoa elimu  
ya uraia kwa wananchi ili nao hatimaye  
waweze kutambua haki zao kwa mujibu  
wa sheria, kuwasilisha madai yao  
mahakamani na kutoa ushahidi pale  
inapobidi kufanya hivyo.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein amefanya uteuzi wa viongozi katika Wizara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ifuatavyo:-

**1. OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

- i. Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi – Dkt. Abdulhamid Y. Mzee
- ii. Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Nd. Salum Maulid Salum
- iii. Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi – Nd. Salmin Amour Abdulla

**2. OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA,  
SERIKALI ZA MITAA NA IDARA  
MAALUM ZA SMZ**

- i. Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Nd. Radhia Rashid Haroub
- ii. Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa , Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Nd. Kai Bushir Mbarouk

**3. OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA,  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA  
BORA**

- i. Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Nd. Asha Ali Abdulla
- ii. Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora anaeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma – Nd. Yakout Hassan Yakout
- iii. Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora anaeshughulikia masuala ya Katiba, Sheria na Utawala Bora – Nd. Kubingwa Mashaka Simba.

**4. OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

- i. Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Nd. Joseph Abdulla Meza
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Nd. Ahmed Kassim Haji

**5. WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango – Nd. Khamis Mussa Omar
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango – Nd. Ali Khamis Juma.

**6. WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA  
MASOKO**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko – Nd. Bakari Haji Bakari

**7. WIZARA YA AFYA**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya – Dkt. Juma Malik Akili
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya – Nd. Halima Maulid Salum
- iii. Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya – Dkt. Jamala Adam Taib

**8. WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA  
AMALI**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali – Nd. Khadija Bakari Juma
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali anaeshughulikia masuala ya Mipango na Uendeshaji - Nd. Abdulla Mzee Abdulla
- iii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali - anaeshughulikia masuala ya Taaluma - Nd. Madina Mjaka Mwinyi

**9. WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA  
MAZINGIRA**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Nd. Ali Khalil Mirza.

**10. WIZARA YA KILIMO, MALIASILI,  
MIFUGO NA UVUVI**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Nd. Juma Ali Juma
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Nd. Maryam Juma Abdulla

**11. WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI,  
WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA  
WATOTO**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto – Nd. Fatma Gharib Bilal
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto – Nd. Maua Makame Rajab

**12. WIZARA YA HABARI, UTALII,  
UTAMADUNI NA MICHEZO**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo – Nd. Omar Hassan Omar
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo – Dkt. Amina Ameir Issa

**13. WIZARA UJENZI, MAWASILIANO NA  
USA FIRISHAJI**

- i. Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Nd. Mustafa Aboud Jumbe
- ii. Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji- Nd. Shomari Omar Shomari

**Uteuzi huo umeanza tarehe 18 Aprili 2016.**

